BEST

MAZINGIRA BORA KWA BIASHARA

# Business Environment Strengthening Programme for Tanzania (BEST)

## Programu ya Kuimarisha na Kuboresha Mazingira ya Biashara

Better Regulation Unit (BRU)

Kitengo cha Kusimamia Sheria na Kanuni Bora

Ofisi ya Raisi, Mipango na Ubinafsishaji

# 1. PROGRAMU YA BEST NI NINI?

- Programu ya BEST ni mpango wa Serikali wa miaka mitano wa kuboresha mazingira ya biashara kwa kupitia sheria na kanuni
  - Madhumuni ni kuongeza mchango na ushiriki wa sekta binafsi (biashara kubwa, biashara ndogo ndogo na hata mtu mmoja mmoja) katika kukuza na kuondoa umaskini.
- Programmu inafadhiliwa na:
  - Serikali ya Tanzania pamoja na
  - Wadau wa maendeleo (DANIDA, DFID, Ubalozi wa Uholanzi na SIDA)

# Komponenti za BEST

Sheria na
Kanuni Bora

Ufumbuzi wa
Migogoro
ya kibishara

**Mazingira Bora**

**Kukua kwa
Sekta binafsi**

**Kukua kwa
Uchumi**

**Kupunguza
umasikini**

Kuimarisha
Kituo cha
Uwekezaji

Kubadili Mila na
desturi za
utendaji wa serikali

Kuongeza ushiriki wa
sekta binafsi –
kufahamu na kudai
mazingira bora

# Maelezo ya Komponenti- BEST

## A: Kuboresha sheria na taratibu

- Lengo Kuu:
  - Kuweka mazingira mazuri ya ushindani wa kibiashara

- Mikakati
  - Kupunguza gharama zisizochangia uzalishaji
  - Kuimarisha ufahamu na uwezo wa utekelezaji wa sheria na kanuni zilizopo na zinazoandaliwa upya
  - Kuweka mfumo utakaohakikisha kuwa sheria na taratibu mpya hazisababishi vikwzo kwa sekta binafsi
  - Kujenga tabia ya sekta binafsi kuitikia matakwa ya taratibu kwa hiari

## A: Kuboresha sheria na taratibu……

- Mbinu zitakazotumika:

  – Kuweka mazingira mazuri ya ushindani wa kibiashara

    Mfano: Mfumo bora wa leseni za Biashara

  - Kupitia na kubadilisha taratibu ambazo ni chanzo dhahiri cha vizuizi vya ukuaji wa sekta binafsi

  - Uchambuzi wa gharama na faida za mapendekezo yanayowasilishwa katika sheria mpya ama zinazobadilishwa na taratibu zinazoendana nazo

  - Utekelezaji madhubuti wa sheria na taratibu zilizopo katika mtizamo wa Serikali (watekelezaji) na sekta binafsi (wahusika)

# Maelezo ya Komponenti –BEST…

## B: Ufumbuzi wa migogoro ya kibiashara …..

Mikakati:

- Kuongeza idadi na kuboresha utumiaji wa mahakama za biashara
- Kurahisisha 'Civil Procedure Code' kama inavyohusu mahakama za Biashara
- Kuimarisha njia mbadala za utatuzi wa migogoro ya biashara
- Kupambana na tabia ya 'injunction/adjournment' kwa kutoa mafunzo kwa Majaji, Mahakimu na Maafisa Wakuu
- Kuharakisha utoaji wa hukumu kwa kesi za biashara
- Utekelezaji wa Mikakati ya Kuzuia Rushwa
- Usuluhishi endelevu na wa haki wa migogoro ya kibiashara
- Marekebisho ya sheria ya udhibiti wa wakala wa mahakama
- Marekebisho ya sheria ya udhibiti wa mawakili

# Maelezo ya Komponenti –BEST..

C: Kuimarisha Kituo cha Uwekezaji Rasilimali

- Malengo Makuu
  - Kuwahudumia wawekezaji kwa kutoa vikwazo vya kibiashara
  - Kuhamasisha uwekezaji hasa kwa SMEs
- Mikakati
  - Kuelezea sura ya Tanzania kama destination ya wawekezaji
  - Kuisaidia serikali kuondoa vizuizi dhidi ya uwekezaji
  - Kuvutia na kuchochea uwekezaji kutoka Nje (FDI)
  - Kuwahudumia wawekezaji waliopo nchini (One stop shop facilitation)
  - Kuendeleza utafiti wa kubaini vikwazo vilivyopo dhidi ya uwekezaji na kutafuta ufumbuzi wa kudumu
  - Kuhamasisha na kuwezesha wawekezaji wadogo kushiriki katika shughuli za kiuchumi

# Maelezo ya Komponenti-BEST..

D: Kubadili mila na desturi za utendaji wa serikali

## Lengo Kuu

- Kuwabadilisha watendaji serikalini kuilea na kuiwezesha sekta binafsi kama mshiriki wa maendeleo na chanzo cha pato la Taifa

## Mikakati

- Mfumo wa huduma ulio wazi kwa watendaji wa sekta ya umma na wa sekta binafsi
- Ushirikishaji wa wadau wote katika (pamoja na sekta binafsi) katika maandalizi na utekelezaji wa sera, sheria na kanuni
- Uchambuzi yakinifu wa sheria na taratibu kabla hazijapitishwa 'Regulatory impact assessment' [RIA]
- Udhibiti wa wenyewe kwa wenyewe ndani ya sekta binafsi (self regulation through codes of conduct)

# Maelezo ya Komponenti-BEST…

E: Kuongeza ushiriki wa sekta binafsi – kufahamu na kudai mazingira bora

Malengo ni:

- Kusaidia uanzishaji na uimarishaji wa taasisi mpya za sekta binafsi
- Kuimarisha asasi za sekta binafsi zinazohusika na masuala ya 'advocacy'
- Kuwezesha asasi za sekta binafsi kutambua matatizo na kudai mazingira bora na kutoa huduma bora zaidi kwa wanachama wake

# Mfumo wa utekelezaji wa BEST

- Programmu iko chini ya Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji
- Kitengo cha Utekelezaji kijulikanacho kama ‘Better Regulation Unit’ Kimeundwa kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Programmu
- Programmu inatekelezwa kwa njia ya ushirikishwaji ikiwahusisha serikali, sekta binafsi na wadau wengine

# Mfumo wa utekelezaji wa BEST…

- Utekelezaji wa komponenti umegawanywa kitaasisi
- Komponenti 4 zinatekelezwa na serikali
- Komponenti 1 (Private Sector Advocacy) inatekelezwa na sekta binafsi

# 2. MALENGO YA BEST KATIKA KUKUZA UCHUMI NA KUONDOA UMASKINI

- BEST ina mchango mkubwa katika kukuza na kuondoa umaskini kwa
  - Kuboresha mazingira ya kufanya biashara
  - Kuongeza ushiriki wa sekta binafsi

↓

BEST inatafsiri kwa vitendo adhma ya serikali ya kuweka mazingira bora ya kufanya biashara na hatimaye kukuza uwezo wa sekta binafsi

- Sheria na kanuni bora, kuinua uwezo wa sekta binafsi wa kutambua na kudai, kuondoa/kupunguza ukiritimba binafsi, kuziwezesha biashara ndogo ndogo

↓

Kukuza Uchumi - Serikali kukusanya kodi zaidi - kutoa huduma bora zaidi – kupunguza umasikini

# 3. VIGEZO VYA MATOKEO YA BEST

- Sheria, taratibu na kanuni bora zipo na zinafanya kazi
- Sekta binafsi inashiriki na kuwakilisha mahitaji yake ki – sera, sheria, taratibu na kanuni katika ngazi zote za serikali
- Kupima ukuaji wa biashara na ongezeko la SMEs
- Kupima ongenzeko ya biashara zinazofuata taratibu
- Kupungua kwa gharama za ufanyaji biashara

# VIGEZO VYA MATOKEO YA BEST……

- Uharaka wa kutatuliwa kwa migogoro ya kibiashara ikiwepo ile ya ardhi n.k.
- Ongezeko la ushiriki wa Sekta binafsi katika shughuli za uchumi na kuondoa umaskini
- Upatikanaji wa masoko na mikopo rahisi/nafuu kwa wafanyabiashara
- Kuongezeka kwa uwekezaji (wa ndani/nje) katika wilaya, mikoa na Tanzania kwa ujumla